

**MUHULA WA PILI 2023**  
**KISWAHILI**  
**KARATASI YA KWANZA (102/1)**  
**KIDATO CHA TATU (3)**  
**MUDA: SAA 2 ½**

**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

**1. Sura ya kumbukumbu iwe na;**

- Mada/kichwa. Kiandikwe kikamilfu.
- Waliohudhuria.
- Waliotuma udhuru.
- Waliokosa bila kutuma udhuru.
- Waalikwa/wageni (kama walikuwamo).
- Ajenda.
- Kufungua mkutano.
- Kusoma na kuthibitisha kumbukumbu za mkutano uliopita.
- Yaliyotokana na kumbukumbu za awali/masuala ibuka.
- Kumbukumbu za mkutano wenyewe zifuate.
- Shughuli nyinginezo/ za ziada.
- Kufunga mkutano.
- Sehemu ya thibitisho la mwenyekiti na katibu. Isitiwe sahihi

**Ajenda zilenge:**

- Masuala ya chama cha Kiswahili.
- miradi/ mipango ya chama

**2. Mtahiniwa ajifunge katika athari mbaya/ madhara ya simutamba miongoni mwa wanafunzi.**

Baadhi ya madhara ni:

- i. wizi wa mtihani
- ii. kuchukua muda mwingi katika mtandao badala ya kusoma
- iii. wanafunzi kutembelea tovuti zisizofaa/ chafu/ upotofu wa maadili.
- iv. wanafunzi kuwasiliana na watu wenye mienendo mibaya
- v. wizi wa simu hizo miongoni mwao
- vi. kutumia pesa nyingi kununua muda wa maongezi
- vii. madhara ya kiafya kutokana na matumizi ya muda mrefu (kadiria)

**3. Hii ni methali**

Alenge maana kuwa atupaye jiwe kuliko na watu wengi hajui litampiga nani.

Huenda likamuumiza mtu wao. Si vyema kufanya kitu cha kuumiza wengi.

Tanbihi

- i) si lazima aeleze maana wala matumizi ya methali.
- ii) Akiandika visa vingi amepotoka kimtindo.

- iii) Lazima pande zote mbili za methali zishughulikiwe. Akishughulikia upande mmoja asipate zaidi ya (C+) (alama 10)
- iv) Aandike kurejelea kila upande wa methali.

#### 4. Insha ya mdokezo

- i) Kisa kioane na mwisho aliopewa.
- ii) Asichopeke tu mwisho huu.
- iii) Kisa kidhihirishe alivyotendewa wema na mtu na akatamani kumwona.
- ii) Kisa lazima kiwe katika nafsi ya kwanza.
- iii) Akikosa kumaliza kwa dondoo, atakuwa amepungukiwa kimaudhui kwa kiasi kikubwa.

### Kutuza

#### Kiwango Alama

- D-01-02 - amejitungia swali  
- haeleweki kwa vyovyote
- D 03 - Anapotoka, lugha hafifu sana
- D+ 04-05 - Insha inaeleweka kwa utata mkubwa  
- makosa mengi ya sarufi, hijai, msamiati na uakifishaji.
- C- 06 - 07 - Japo anajaribu kujibu swali ana makosa mengi ya sarufi, na hijai msamiati na uakifishaji
- C 08 - Makosa mengi ya sarufi, hijai, msamiati na uakifishaji  
- Mada haikuzwi kilcamilifu  
- Hana ubunifu wa kutosha
- C+ 09-10 - Licha ya makosa ya sarufi, hijai, msamiati na uakifishaji anaeleweka.  
- Anatomia tamathali za usemi kwa njia halifu
- B- 11- 12 - amezingatia mada kikamilifu. Ana makosa ya hijai, na msamiati. Ana machache ya uakifishaji.
- B 1 3 - Amezingatia mada kikamilifu. Lugha ya mnato imeanza kujitokeza  
- makosa ni machache ya hapa na pale
- B+ 14- 15 - Amejibu swali kikamilifu. Ametunijia lugha ya mnato.  
- makosa machache ya sarufi hijai, na msamiati.
- A- 16- 17 - Anaibua hoja zilizokomaa.  
Lugha yakeni ya kuvutia mno.  
- Amezingatia urefu  
- Anatomia mitindo mbalimbali ya sentensi  
- Uakifishaji wake ni mzuri zaidi. Makosa ni machache sana yasiyokusudiwa.
- A 18 - makosâ yote yasizidi matano.
- A+ 19- 20 - Insha ni nzuri mno. Haina makosa ya ama yoyote.